**Jina** .............................................................................................. **Namba yako** ....................................

102/2
**KISWAHILI**
Karatasi 2
Okitoba/Novemba 2015
**Muda: Saa 2½**

Sahihi ya Mtahiniwa ........................................

Tarehe ........................................................

# TATHMINI YA PAMOJA YA KAUNTI NDOGO YA KANDARA KIDATO CHA TATU

Hati ya kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya Kidato cha Tatu.

**KISWAHILI**
Karatasi 2
Octoba/Novemba 2015
**Muda: Saa 2½**

## MAAGIZO KWA MTAHINIWA

- Andika jina lako ya namba yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
- Jibu maswali yote. Majibu yako yaandikwe katika nafasi zilizoachwa katika kiji tabu hiki cha maswali.

**Kwa matumizi ya mtahini**

| Swali | Alama | Tuzo |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| **Jumla** | **100** | |

**SEHEMU A: Ufahamu** **(alama 15)**

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.

Jinsi Kiswahili kinavyozidi kuzungumzwa na watu wengi ndivyo kinavyozidi kuingilia lugha nyingine za Kiafrika. Katika miji, kwa mfano, watoto wengi wanajifunza Kiswahili wakiwa bado wadogo sana na kwa wengi, lugha hii inakuwa ndiyo lugha ya asili. Hata ikiwa wataelewa lugha za wazazi wao, bado matumizi ya Kiswahili yanabaki kuwa mapana zaidi. Wazazi wengi hutumia Kiswahili nyumbani kwao hasa ikiwa wametoka makabila tofauti. Ni vigumu sana kumskia mtu yeyote akizungumza lugha yake ya kwanza bila ya kusikia maneno kadha wa kadha ya Kiswahili. Mengine ni maneno ya kawaida sana ambayo tunaweza kusema lazima yapo kwenye msamiati wa lugha yoyote bila ya hata kukopwa kutoka Kiswahili. Wala uhusiano huo si wa upande mmoja tu. Lazima tutarajie kwamba lugha za makabila ya watu wote hawa ambao wanaongea Kiswahili (kama lugha ya pili) **zitajipenyeza** katika Kiswahili.

Tofauti kubwa tunayoiona kati ya wazungumzaji wa Kiswahili wanaotoka bara na wale wa pwani ni katika **matamshi.** Ndiyo maana watu wengi hutambulika upesi mahali **wanapotoka** mara tu wanapofungua midomo yao kuzungumza Kiswahili. Kwa hivyo, mtu anayesema: Habari ya asubuhi bwana; Nakutakia heli; Hadisi hii imenifulahisha; Najiona zaifu sana; Huyu ni njomba wangu......na kadhalika, anaweza kuambiwa labda huyo ni 'mshamba'.

Kuna mifano mingi ya aina hiyo inayoweza kutolewa. Kuifafanua lazima tuwe na maelezo kamili kuhusu fonolojia za lugha za wazungumzaji. Kiswahi kima maingiliano na lugha nyingine na vilugha vya 'zamani' vya Kiswahili. Pia kuna vilugha vingi vya Kiswahili vinavyozuka hivi sasa ambavyo havijafikiriwa kufanyiwa **uchunguzi**. Watu wamesikika wakisema; Achana naye maze buda huyo; madem wa hapa wamededi; Tuliambiwa ameswichi; na kadhalika.

Kwa sababu Kiswahili kinazungumzwa na watu wengi zaidi kutoka sehemu mbalimbali za Afrika Mashariki, Lazima kutaonekana tofauti kutokana na lugha ya asili ya kila mtu. Ingawaje ni kweli kuwa shuleni walimu wanajitahidi kufunza Kiswahili sanifu, matumizi ~~ya aina hii ya Kiswahili yana mipaka~~ yake.

Tunaweza hata kusema kuwa lugha yoyote inayoitwa 'sanifu' haina wazungumzaji asilia bali ni lugha ambayo inakubalika kutumika kwa madhumuni maalum, na kazi yake ni kuunganisha vilugha vyote na vijilugha vya aina hiyo. Yaani ni kama lugha sanifu ni kilugha kimojawapo cha lugha hiyo ambacho kila mzungumzaji wa lugha hiyo anapaswa kukijua. Kwa upande wa Kiswahili, kila msemaji anapaswa kukijua Kiswahili sanifu ili kuelewa taarifa za habari redioni, magazetini na pia kuelewana na wananchi kutoka sehemu zingine za nchi.

**Maswali:**

**a)** Kiswahili sanifu kina uwezo gani? (alama 2)

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

**b)** Taja mambo mawili ambayo yameikumba lugha ya Kiswahili katika harakati ya kukua kwake. (alama 2)

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

c) Taja aina mbili za lugha kama zilivyoelezewa na matamshi yaliyopendekezwa. (alama 2)

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

d) Andika dosari zifuatazo za matamishi zilizoko katika kifungu katika lugha sanifu. (alama 2)

i) Habari ya asubuhi bwana.
ii) Madam wa hapa wamededi

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

e) Taja mambo yanayothibitisha kukua kwa Kiswahili. (alama 3)

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika kifungu. (alama 4)

i) Matamshi

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

ii) Kupotoka

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

iii)Uchunguzi

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

iv)Zitajipenyeza

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

**SEHEMU B: Mmuhtasari** **(Alama 15)**

Soma habari kisha ujibu maswali yafuatayo.

Tetekuwanga ni mojawapo ya magonjwa yanayowasumbua watoto wachanga. Huu ni ugonjwa ambao kila mzazi hutazamia mtoto wake augue. Wataalam wa afya husema kuwa ni lazima kila mtu augue ugonjwa huu mara moja maishani. Asipougua akiwa mtoto, utampata akiwa.mtu mzima.

Ni muhimu kihakikisha kuwa watoto wamekingwa dhidi ya ugonjwa huu. Kuna chanjo ya kukinga mtoto dhidi ya tetekuwanga tofauti na zamani ambapo uliwaua watoto wengi. Maradhi haya husababisha vipele mwilini mwa mtoto, ngozi huwasha na baadaye vidonda vilivyo na umajimaji hutokezea mwilini. Ugonjwa huu huenea kwa haraka sana.

Mtu anaweza kuambukizwa tetekuwanga kwa kushika kidonda au ngozi ya mtu anayeugua. Pia mtu anayeugua akipiga chafya au kukohoa anaweza kuwaambukiza wengine virusi vya tetekuwanga. Maradhi haya hujitokeza katika muda wa siku ishirini na moja baada ya kuambukizwa. Watoto wengi ambao huambukizwa huwa chini ya miaka kumi. Watoto waliopata chanjo ya kuzuia ugonjwa huu hawawezi kuupata kabla ya kufikisha umri wa mwaka mmoja. Hii ni kwa sababu chembechembe za damu ya mama huwasaidia kuimarisha kinga dhidi ya ugonjwa huu. Watoto ambao wana kinga hafifu ya mwili wanaweza kulemewa.

Hapo mbeleni ugonjwa huu ulienea sana lakini sasa kuna chanjo iliyoimarishwa ya kuudhibiti. Athari za ugonjwa huu kwa watoto huwa ni mbaya sana. Kuugua tetekuwanga katika utu uzima kuna athari zake ambazo zaweza kuwa mbaya zaidi.

Dalili za ugonjwa huu hazifai kupuuzwa, nazo ni: homa, maumivu ya tumbo na kukosa hamu ya kula. Mgonjwa pia anaweza kuhisi maumivu ya kichwa na mwili. Mtoto huwa na vidonda vidogovidogo vyekundu vilivyojaa umajimaji. Hata hivyo, vidonda hivyo haviachi kovu mwilini vinapopona ikiwa havikupata bacteria hatari. Watoto waliochanjwa mapema dhidi ya ugonjwa huu hupona haraka wauguapo kuliko wale ambao hawakuchanjwa. Mtoto ambaye ana tetekuwanga anafaa azuiwe kukuna vidonda kwa vile anaweza kuathiriwa zaidi au akawa na uchungu. Ni vizuri kutovifunika vidonda kwa sababu vinaweza kuwa vibaya zaidi.

Maswali

**a)** Fupisha aya mbili za kwanza (maneno 45 - 50) (alama 6, 1 mtiririko)

Matayarisho

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

Jibu

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

**b)** Fupisha aya tatu za mwisho (maneno 70 - 80) (alama 7, 1 mtiririko)

Matayarisho

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

Jibu

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

**MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)**

**a)** Bainisha vielezi katika sentensi zifuatazo kasha ueleze ni vya aina gani. (alama 2)

i) Rubani aliendesha ndege kistadi

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

ii) Wachezaji wamo uwanjani

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

**b)** Onyesha virai katika sentensi hii. (alama 2)
Mkulima Yule amelima vizuri sana.

.................................................................................................................................................

.................................................................................................................................................

**c)** Ainisha vitenzi katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
Huyu ndiye daktari aliyekuwa akinitibu.

.................................................................................................................................................

.................................................................................................................................................

**d)** Tambua aina za shamirisho katika sentensi hii. (alama 2)
Kocha alimrushia kijana mpira

.................................................................................................................................................

.................................................................................................................................................

**e)** Andika katika hali yakinishi. (alama 2)
Tafadhali usimwazime kalamu hatakurudishia

.................................................................................................................................................

.................................................................................................................................................

**f)** Tumia kirejeshi 'o' tamati katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
Cheo ambacho anapewa ni kile ambacho anakitaka.

.................................................................................................................................................

.................................................................................................................................................

**g)** Bainisha mwingiliano wa maneno katika sentensi ifuatayo. (alaama 2)
Alipofika alifahamu Fika kuwa ameanguka mtihani.

.................................................................................................................................................

.................................................................................................................................................

**h)** Andika sentensi ifuatayo katika haliya udogo wingi. (alama 2)
Mbuzi wa mkulima huyu amevunjika mguu.

.................................................................................................................................................

.................................................................................................................................................

**i)** Bainisha vishazi katika sentensi hii. (alama 2)
Mara tu walipowasili walipewa zawadi zao.

.................................................................................................................................................

.................................................................................................................................................

**j)** Changanua sentensi ifuatayo kwa mishale. (alama 4)
Mama na mtoto walienda mjini.

.................................................................................................................................................

.................................................................................................................................................

.................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

**k)** **Akifisha** sentensi hii: (alama 2)
Niletee gazeti la daily nation mwalimu alisema.

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

**l)** Onyesha ngeli za maneno yafuatayo. (alama 2)

i) Waraka

..............................................................................................................................................

ii) kipofu

..............................................................................................................................................

**m)** Taja sauti mbili za meyoni. (alama 2)

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

**n)** **Ainisha viambishi**
Alichezesha

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

**o)** Andika upya sentensi ifuatayo ukizingatia kinyume cha maneno yaliyopigiwa mstari. (alama 2)
<u>Aliandika</u> maandishi <u>yaliyobandikwa</u>

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

**p)** Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizo kwenye mabano. (alama 2)

i) nywa (tendesha) ..............................................................................................................

ii) vaa (tendwa) ..................................................................................................................

**q)** Bainisha kiima na chagizo katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
Wanafunzi hao walisoma maswali yote kwa makini.

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

r) Eleza matumizi mawili ya kikomo. (alama 2)

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

s) Tumia neno sasa kutofautisha kati ya silabi na mofimu. (alama 2)

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

**ISIMUJAMII (Alama 10)**

Muuzaji: Wewe haujambo?

Mteja : Mzuri sana.

Muuzaji: Unataka nini?

Mteja: Mimi nataka majani ya kupikia chai.

Muuzaji: Majani iko hapa na kwa bei mzuri.

Mteja: Inaitwaje

Muuzaji: Inaitwa ketepa

**Maswali**

a) Hii ni sajili gani? (alama 2)

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

b) Eleza sifa nne za sajili hiyo. (alama 8)

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................